*Namba ya Mtahiniwa*_________________________________

*Jina la Shule*_________________________________

# KEYS EDUCATIONAL AND STATIONERY SERVICES (KESS)

## NAMBA YA USAJILI: 473801

Barua pepe: keyseducationalservices@gmail.com

**Simu: 0758587618/0679587618**

KIFURU-KINYEREZI, DAR ES SALAAM

# MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU DARASA LA SABA

## 01: KISWAHILI

**Muda: Saa 1:30** **Ijumaa Machi 8, 2024**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu **A, B,** na **C** zenye jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii
4. Tumia kalamu ya wino wa rangi ya **buluu** au **mweusi**
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Jina lako** na **Jina la Shule** sehemu ya juu kulia kwenye kona ya kila ukurasa

| **KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU** | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **JINA LA MTAHINI** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MWINGIZA ALAMA** | | |
| **SAINI YA MHAKIKI** | | |

*Namba ya Mtahiniwa*__________________________

*Jina la Shule*____________________________________

**SEHEMU A (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamizi. Kisha jibu kipengele cha (i) – (v), **kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika mabano**

i. Kijiji cha Manungu kilikuwa karibu na nini?
A. Mto B. Msitu C. Pori D. Bahari E. Mlima [ ]

ii. Mzee Jojo alisifika kwa kilimo cha nini?
A. Chai B. Buni C. Zabibu D. Ndizi E. Karafuu [ ]

iii. Wanyama gani walikuwa wanakula ndizi shambani kwa mzee Jojo?
A. Nzige B. Nguruwe C. Ngedere D. Sokwe E. Tembo [ ]

iv. Nani walimfyatulia risasi Dunga?
A. Wanajeshi C. Mzee Jojo E. Wakulima
B. Wanakiji cha Manungu D. Walinzi [ ]

v. Nahau "kuponea chupu chupu" kama ilivyotumika katika hadithi uliyoisikia ina maana gani?
A. Kufariki B. Kukamatwa C. Kuumizwa D. Kupigwa E. Kunusurika [ ]

2. **Katika kipengele cha (i) – (x), chagua jibu sahihi kutoka kwenye machaguo na kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye mabano.**

i. Amekula ingawa hajatosheka kabisa. Katika sentensi hii neno lipi limetumika kama kiungo?
A. Amekula B. Ingawa C. Hajatosheeka D. Kabisa E. Hajala [ ]

ii. Ninyi mnakula chakula. Sentensi hii ipo katika nafsi ipi?
A. Nafsi ya kwanza umoja C. Nafsi ya tatu umoja E. Nafsi ya tatu wingi
B. Nafsi ya pili umoja D. Nafsi ya pili wingi [ ]

iii. Lipi kati ya haya yafuatayo ni jibu la kitendawili: Nina mdomo lakini sina mikono wala miguu?
A. Jongoo B. Nyoka C. Ulimi D. Macho E. Utumbo [ ]

iv. "Nendeni nyumbani upesi" Mama alisema. Sentensi hii ipo katika kauli gani?
A. Tata B. Halisi C. Mazoea D. Taarifa E. Jumuishi [ ]

v. Methali hakuna marefu yasiyo na ncha ina maana gani?
A. Hakuna jambo lenye mwanzo mrefu D. Hakuna jambo lisilokuwa na mwisho
B. Hakuna kitu kisicho kirefu E. Hakuna jambo lenye mwanzo na mwisho [ ]
C. Shida siyo ya mtu mmoja

vi. Mtama umeliwa na ndege. Neno "umeliwa" linaonesha kauli ipi ya utendaji?
A. Kutenda B. Kutendea C. Kutendwa D. Kutendeka E. Kutendewa [ ]

vii. Neno lipi ni tofauti na maneno mengine kati ya maneno haya?
A. Kambare B. Kaa C. Perege D. Sangara E. Kibua [ ]

viii. Rais alisisitiza kuwa kila mtanzania hana budi <u>kufanya kazi kwa bidii</u> ili kuieletea nchi yetu maendeleo. Nahau ipi ina maana sawa na kifungu cha maneno kilichopigiwa mstari?
A. Kufanya kazi bega kwa bega C. Kuchapa kazi E. Kukata shauri [ ]
B. Kupiga uvivu D. Kupiga maji

ix. Shamba langu kubwa lina kisiki kimoja. Jibu la kitendawili hiki ni lipi?
A. Nywele B. Nyota na mwezi C. Tumbo na kitovu D. Ulimi na meno E. Kinywa na ulimi [ ]

x. Kamilisha methali hii: Nzi kufa juu ya kidonda__________________________
A. Ni vizuri C. Si haramu E. Ni ujinga
B. Si kupenda D. Ni heri kuliko kupigwa [ ]

*Namba ya Mtahiniwa*_________________________

*Jina la Shule*__________________________________

3. Oanisha maneno yaliyopo katika **KIFUNGU A** na yale ya **KIFUNGU B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika mabano

| KIFUNGU A | MAJIBU | KIFUNGU B |
|---|---|---|
| i. Tabia ya mtu kutopenda mafanikio ya mtu mwingine | [ ] | A. Dafina |
| ii. Bakiza sehemu ya kitu unachotumia au unachokichukua | [ ] | B. Fichama |
| iii. Mali iliyofukiwa chini ya ardhi kwa lengo la kufichwa | [ ] | C. Fuadi |
| iv. Jambo kubwa la heshima na fahari | [ ] | D. Inda |
| v. Kufika mwisho au kikomo cha jambo | [ ] | E. Kaditama |
| | | F. Adhama |
| | | G. Saza |

**SEHEMU B (Alama 20)**

4. Umepewa sentensi tano ambazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko ulio sahihi kwa kuzipa herufi A**, B, C, D na E** ili kuunda kifungu cha habari.

i. Baadaye, wazazi wake walihamia Zanzibar angali bado akiwa mtoto mdogo. [ ]
ii. Alifariki tarehe 29 Februari 2024 katika hospitali ya Mzena iliyopo jijini Dar es salaam. [ ]
iii. Alizaliwa tarehe 8, Mei 1925 katika kijiji cha Kivule wilayani Mkuranga Mkoani Pwani. [ ]
iv. Ali Hassani Mwinyi alikuwa Rais wa awamu ya pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1985-1995. [ ]
v. Alisoma shule ya Msingi Mangapwani iliyopo huko Unguja, Zanzibar [ ]

5. **Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika sehemu zilizoachwa wazi**

Bwana na Bibi Pondamali waliishi muda mrefu bila kupata mtoto. Hali hii iliwahuzunisha sana. Kila mara walipowaona watoto wa wenzao, waliumia. Walitamani na wao wapate mtoto. Mke wa Bwana Pondamali ndiye aliyekuwa na simanzi zaidi. Kila siku alijiuliza lini atapata mtoto.

Siku moja, wakati mke wa Bwana Pondamali akiwa amejiinamia, mumewe alimshika bega na kumuuliza, “Mke wangu, mbona uko katika lindi la mawazo?” Mke wake hakumjibu. Aliendelea kujiinamia. Mumewe alimsihi kutokuwa na mawazo kila wakati.

Bwana na Bibi Pondamali waliendelea kumwomba Mungu ili wapate mtoto kwani waliamini kuwa mwomba Mungu hachoki. Pia, subira yavuta heri. Hatimaye, wakati ulifika ambapo Bwana na Bibi Pondamali walipata mtoto wa kike ambaye walimpa jina la Subira.

Subira alilelewa kwa mapenzi makubwa. Wazazi wake walimpatia kila alichohitaji. Pia, walimdekeza kupita kiasi. Subira alikua akawa msichana mkubwa. Kutokana na malezi aliyopewa na wazazi wake, Subira hakuwa na tabia nzuri. Tabia yake iliwakera wengi katika eneo waliloishi kwani ilikiuka maadili ya jamii kwa ujumla.

Namba ya Mtahiniwa___________________________
*Jina la Shule*_____________________________________

**Maswali**

i. Kipi kiliwahuzunisha Bwana na Bibi Pondamali?
_______________________________________________________________________________________

ii. Nani aliyekuwa na simanzi zaidi?
_______________________________________________________________________________________

iii. Kwanini Subira hakuwa na tabia nzuri?
_______________________________________________________________________________________

iv. Neno lipi lina maana sawa na neno simanzi kama lilivyotumika katika habari uliyoisikia?
_______________________________________________________________________________________

v. Je, ni funzo gani unalipata kutokana na kifungu cha habari hapo juu?
_______________________________________________________________________________________

**SEHHEMU C: (Alama 10)**

6. Bainisha vipengele vya barua ya kiofisi ifuatayo kwa kuandika majibu sahihi katika sehemu zilizoachwa wazi

Kijiji cha Kitunga,
S. L. P. 18,
**Magonde.**
i._____________

ii. ___________________________

Meneja wa Kiwanda,
Kiwanda cha Saruji Dondwe,
S.L.P. 79,
**Kipote.**

Ndugu,

iii.________________________________________________________________

Husika na kichwa cha barua hii hapo juu. Ninayo heshima kubwa ya kuomba kazi ya uhasibu kama ilivyotangazwa na Kampuni yako kupitia gazeti la Kipepeo Toleo Na. 08 la tarehe 28 Februari 2024. Ninayo elimu na uzoefu wa kutosha katika kazi hiyo kwani nimewahi kufanya kazi katika makampuni mbalimbali kwa mafanikio makubwa

iv.____________________________________________________________

v.____________________________________________________

Kimea Mbena